
# Mambo 101 Unayohitaji Kuyafahamu Kuhusu Polisi Lakini Unaogopa Kuyauliza




Commonwealth Human Rights Initiative

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

British High Commission Dar es Salaam

Kijitabu hiki kimetayarishwa na:
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: http://www.chragg.go.tz

Kwa ushirikiano na:
Taasisi ya Jumuiya ya Madola ya Masuala ya Haki za Binadamu
(Commonwealth Human Rights Initiative)
B-117, Iind Floor, Sarvodaya Enclave, New Delhi – 110 017
Simu: +91 –(0)11 4318 0200
Faksi: +91 –(0)11 2686 4688
Barua Pepe: info@humanrightsinitiave.org
Tovuti: www.humanrightsinitiative.org

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni taasisi huru ya Serikali, iliyoanzishwa kama taasisi ya kitaifa iliyo kitovu cha kukuza na kulinda haki za binadamu na wajibu na utawala bora nchini Tanzania. THBUB ilianzishwa chini ya ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na ilianza kazi tarehe 1 Julai, 2001 baada ya kupitishwa kwa Sheria Na. 7 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001. Tume ina majukumu ya kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kutoa mapendekezo, ikibidi inaweza kupeleka masuala hayo mahakamani. Pia Tume hutoa mapendekezo kwa ajili ya kuboresha sheria na kanuni zilizopo au miswada ya sheria na kanuni au taratibu za kiutawala ili kuhakikisha kuwa haki za binadamu na utawala bora vinazingatiwa. Tume inafanyakazi Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar. Kwa hivi sasa ina ofisi nne zilizoko Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi na Mwanza.

Mradi wa Masuala ya Haki za Binadamu wa Taasisi ya Jumuiya ya Madola (CHRI) ni taasisi ya kimataifa isiyo ya Serikali iliyo huru na isiyofungamana na upande wowote, yenye jukumu la kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinakuwepo na zinaheshimiwa katika nchi zote za jumuiya ya madola. CHRI ilianzishwa mwaka 1987 na vyama vya wanataaluma wa nchi za jumuiya ya madola; ina makao yake makuu New Delhi, India na ina ofisi zake Accra, Ghana na London, Uingereza. CHRI inasimamia ulinzi na ukuzaji wa sheria za kimataifa za haki za binadamu na uzingatiaji wa kanuni za nchi za jumuiya za madola za Harare. Masuala yanayohusiana na uwajibikaji na ushirikishwaji katika utawala – fursa ya kupata haki na fursa ya kupata taarifa – ndicho kiini cha kazi za CHRI. Pia CHRI inajishughulisha na kutoa picha ya jumla ya hali ya haki za binadamu katika nchi za jumuiya ya madola, ikiangalia zaidi masuala ya watetezi wa haki za binadamu, uzingatiaji wa matakwa ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa unaofanywa na nchi za jumuiya ya madola.

THBUB na CHRI wanatambua mchango mkubwa wa Jeshi la Polisi Tanzania katika kuandaa kijitabu hiki.

Taarifa iliyomo katika kijitabu hiki inaweza kutumiwa na mtu au taasisi yoyote kwa kukitambua chanzo cha taarifa.

Ubunifu na: Aspire Design, New Delhi
Vielelezo na: Fahad Faizal
Kimechapwa na: Jamana Printers Limited, Tanzania.

Kwa ufadhili wa:
Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania.

2013

British
High Commission
Dar es Salaam

# Mambo 101 Unayohitaji Kuyafahamu Kuhusu Polisi Lakini Unaogopa Kuyauliza



# Utangulizi

Tunakutana na Polisi kila siku, na tunawaona wakifanya kazi nyingi, kama vile kuongoza magari, kuwalinda viongozi, kudhibiti mikusanyiko ya watu, kusindikiza watuhumiwa mahakamani, kufanya upelelezi, kutoa ushahidi mahakamani, kupokea malalamiko vituoni, kubaini, kuzuia au kukamata wahalifu, kupambana na wahalifu na kazi nyinginezo nyingi. Pia tumesikia na tunaendelea kusikia mengi kuhusu polisi kupitia magazeti, televisheni, radio na maneno ya watu. Aidha, kila mtu ana mtazamo wake juu ya polisi. Hata hivyo, watu wengi bado wanauelewa mdogo sana kuhusu Polisi.

Katika nchi yenye demokrasia polisi siyo wakala wa serikali iliyopo madarakani wanao vaa sare zao ili kuwakandamiza wananchi na kuwadhibiti. Kwa kiwango fulani Polisi wanafanana na kikosi cha zimamoto au mamlaka ya kodi ya mapato, kwani wanatoa huduma muhimu ambazo kisheria zina jukumu la kumlinda na kumwangalia kila mmoja wetu.

Kwa kadiri polisi walivyo na wajibu kwa wananchi, nao wananchi wanao wajibu kwa polisi. Raia wema wenye kuwajibika hawapaswi kuwaogopa na kuwachukia polisi au kuogopa kwenda kituo cha polisi pale wanapokuwa na matatizo. Bali wananchi na polisi wanatakiwa wafanyekazi pamoja katika kuzilinda sheria.

Hivyo basi, ni muhimu kuzielewa kazi za polisi, jinsi wanavyozifanya na changamoto wanazokumbana nazo. Pia ni muhimu kujua jinsi taasisi hii inavyoonekana na ukomo wa madaraka na kazi zao. Aidha, ni muhimu kwetu sisi kujua haki na wajibu wetu ili pasiwepo mtu yeyote si polisi wala raia atakayevunja sheria pasipo kuchukuliwa hatua yoyote. Na hii ndiyo maana halisi ya utawala wa sheria.

Kijitabu hiki ni mwongozo kwa wewe kuijua polisi. Ni kwa kuijua vizuri polisi tu ndipo tunapoweza kuongea kwa kujiamini, na kukemea maovu yanayojitokeza katika jamii yetu, na kwa kufanya hivyo hali ya mambo itabadilika. Kijitabu hiki kimechapishwa na kuletwa kwako kwa matumaini kuwa kitakusaidia kujua mambo mbalimbali kuhusu polisi na kazi zao na utatumia elimu hiyo kudai huduma bora za kipolisi ambazo wote tunastahili kupata.

## 1. PT ni nini?

PT ni kifupi cha Polisi Tanzania. Ni chombo cha muungano wa Tanzania kilichoundwa ili kuwahakikishia wananchi usalama wao na mali zao, kudumisha amani na utulivu katika jamii, pia kuzuia, kubaini na kupambana na uhalifu. Ni chombo cha Serikali kilichopewa mamlaka na wajibu wa kuajiri, na kuwapangia askari polisi vituo vya kufanyia kazi na kuratibu masuala yote ya amani na utulivu ndani ya nchi.

## 2. Kwanini tuna Jeshi la Polisi?

Jeshi la Polisi lipo kwa lengo la kuwahakikishia wananchi usalama wao na mali zao, kudumisha amani na utulivu katika jamii, pia kuzuia, kubaini na kupambana na uhalifu. Jeshi la Polisi lipo kama sheria inavyoelekeza kuhakikisha kuwa kila mtu, wakiwemo askari polisi wanafuata sheria katika kila hatua.



## 3. Jeshi la Polisi linapaswa kufanya nini?

Jeshi la Polisi lina kazi kadhaa: lazima lizuie na kudhibiti uhalifu, libaini na kuchunguza vizuri wakati wowote uhalifu unapotokea. Pia ni lazima litayarishe shauri la kweli na lenye ushahidi ili Mwendesha mashtaka aweze kuwasilisha mahakamani. Jeshi la polisi lina jukumu la kudumisha sheria na utulivu na ili kutimiza azma hii linakusanya taarifa kuhusu kinachotokea katika jamii inayoihudumia.



## 4. Nini maana ya mamlaka ya polisi?

Jeshi la Polisi lina mamlaka mbalimbali yaliyotolewa kisheria na linapaswa kutumia mamlaka hayo kulingana na taratibu zilizoainishwa katika sheria husika. Hivyo polisi wanaweza kukamata, kufanya upekuzi, kushikilia, kumpeleleza mtuhumiwa, kumhoji shahidi, kufanya mahojiano na mtuhumiwa, kutawanya waandamanaji wenye nia ovu na kuhakikisha usalama katika jamii. Wanatakiwa kufanya hivyo kwa kufuata taratibu zinavyowaelekeza na siyo vinginevyo. Hawawezi kufanya kama wapendavyo. Matumizi yoyote mabaya ya mamlaka au uzembe katika kazi unapelekea utovu wa nidhamu na uhalifu, na afisa wa polisi anayetenda hayo anapaswa kuchukuliwa hatua stahiki. Sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Jeshi la Polisi Na. 322 (Police Force and Auxiliary Service Act 2002 CAP 322) na Kanuni za Polisi (Police General Orders) zimeainisha mamlaka ya polisi.

## 5. Je, kuna Jeshi la Polisi moja tu nchini Tanzania?

Ndiyo, nchini Tanzania kuna Jeshi la Polisi moja lenye vikosi, Idara na vitengo mbalimbali kama vile kikosi cha kutuliza ghasia, kikosi cha usalama barabarani, kikosi cha wanamaji, kikosi maalum cha kuzuia dawa za kulevya, idara ya upelelezi, n.k.



Pia kulingana na Sheria ya Jeshi la Polisi kuna askari polisi wasaidizi ambao wanawasaidia polisi wa kawaida kufanya shughuli zao za kila siku za kusimamia sheria na kulinda mali za wananchi. Afisa wa polisi ana uwezo wa kuamrisha polisi wasaidizi. Polisi wasaidizi wanauwezo wa kipolisi wa kupekua na kukamata na pia wanakinga kama afisa wa polisi. Polisi wasaidizi wakimkamata mtuhumiwa wanawajibika kumkabidhi kwa polisi aliyekaribu

nao au kumpeleka katika kituo cha polisi kilichopo karibu na alipokamatwa mtuhumiwa.

## 6. Je, mtu yeyote anaweza kuwa polisi?

Ndiyo, mtu yeyote anaweza kuwa askari polisi iwapo ametimiza masharti na vigezo vilivyowekwa. Kwa mfano kujiunga na polisi katika ngazi ya chini (konstebo) lazima uwe umehitimu na kufaulu elimu ya kidato cha nne, sita au elimu ya juu au uwe na sifa ya nyongeza ya ujuzi katika taaluma fulani.

## 7. Nawezaje kujiunga na Jeshi la Polisi Tanzania?

Unaweza kujiunga na Jeshi la polisi kwa kutuma maombi kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kama ametoa tangazo la ajira kwa kupitia ofisi za wilaya, mkoa na taifa, au kupitia katika tovuti yao. Hata hivyo hivi karibuni wameanza kuchukua wanafunzi kutoka shuleni moja kwa moja kwa kujaza fomu maalumu. Ukishapeleka maombi utafanya usaili ambapo waliokidhi vigezo wanachaguliwa na kupelekwa kwa ajili ya mafunzo ya awali chuo cha polisi Moshi. Ukishamaliza mafunzo hayo na kufaulu utapangiwa kituo cha kazi.




## 8. Nitapata mafunzo gani kama askari polisi?

Kama askari polisi unahitaji kufundishwa majukumu ya msingi na wajibu wako kama mwanajumuiya ya Jeshi la Polisi Tanzania. Polisi wanapata mafunzo ya awali kwenye chuo cha Polisi Moshi. Kwa wakaguzi na maafisa wa polisi wanapata mafunzo yao kwenye Chuo cha Polisi kilichopo Kurasini Dar es Salaam na Kidatu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya uongozi na utawala. Pia polisi kutokana na vitengo vyao wanapata mafunzo mengine kulingana na majukumu yao.

.

## 9. Je, ni aina gani nyingine ya mafunzo nitapata?

Mafunzo mengine kwa polisi baada ya mafunzo ya msingi yanategemea majukumu na wajibu wa polisi mmoja mmoja na idara aliko, mabadilko ya teknolojia, muda, mahali na mahitaji ya Jeshi la Polisi. Mafunzo yanaweza kuhusu mazoezi ya viungo, matumizi ya silaha, huduma ya kwanza, kudhibiti ghasia na mapambano bila kutumia silaha, sheria ya jinai, taratibu za kazi, namna ya kufanya upelelezi, namna ya kudhibiti umati wa watu na namna ya kufanyakazi katika mazingira mbalimbali wanayokutana nayo. Mengi ya mafunzo haya hutolewa katika vipindi maalumu kupitia programu ya mafunzo kazini kwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.



## 10. Askari polisi anawezaje kupandishwa cheo?

Askari polisi anaweza kupandishwa kwenda cheo cha juu mintarafu ustadi wake kitaaluma, elimu na uzoefu, uwezo wa utendaji kazi, uadilifu na kufaulu mitihani katika programu za mafunzo ya ndani ya Jeshi la Polisi.

Polisi anaweza kupandishwa cheo kwenda ngazi ya ukoplo na sajenti meja kwa kupata mafunzo yanayotolewa katika chuo cha Polisi Moshi na Zanzibar na kwa cheo cha Ukaguzi na Uafisa kwenye chuo cha Polisi Dar es Salaam kilichopo Kurasini. Hata hivyo cheo cha Ukaguzi na Uafisa kinathibitishwa na Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi na Magereza.

**11. Je, kuna vituo vingapi vya polisi nchini?**

Hadi kufikia mwaka 2012 idadi ya vituo vya polisi nchini ilikuwa ni 194 pamoja na vingine vidogo vidogo (outposts). Vituo hivi vipo kwenye mikoa, wilaya, tarafa, kata na sehemu nyingine vijijini, kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi.

**12. Je, uwiano wa askari polisi na wananchi unakidhi mahitaji?**

Idadi ya polisi waliopo nchini haina uwiano na wingi wa watu na mahitaji halisi. Hivi sasa nchini Tanzania askari polisi mmoja anahudumia wastani wa wanachi 1,300 tofauti na viwango vya Umoja wa Mataifa ambapo askari polisi mmoja anatakiwa ahadumie wastani wa wananchi 450. Askari polisi wengi wanatumika kulinda kundi dogo la watu muhimu, au katika utekelezaji wa shughuli za utawala na usalama barabarani. Hii inamaanisha kuwa kuna upungufu mkubwa wa askari polisi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya jeshi hilo.

**13. Jeshi la Polisi lina askari wanawake?**

Ndiyo, Jeshi la Polisi lina askari wanawake, lakini ni wachache. Hivi sasa jeshi la polisi lina askari wanawake wapatao 7,450. Kwahiyo hii inaonyesha kuwa kuna baadhi ya vituo vinaweza visiwe na askari wanawake. Hii inadhihirisha kwamba idadi ya askari wanawake ni ndogo na ipo haja ya idadi hii kuongezwa.

**14. Je, polisi wanawake wana majukumu tofauti?**

Hapana: Hadi sasa kulingana na kanuni na sheria zilizopo polisi wanawake wanatekeleza majukumu sawa na polisi wanaume, pia wanapelekwa kwenye vituo vile vile ambavyo polisi wanaume wanapelekwa na kutekeleza majukumu yaleyale kama vile kitengo cha kutuliza ghasia (FFU), kitengo cha upelelezi, kitengo cha mbwa na farasi, kikosi cha wanamaji, chuoni n.k.

**15. Je, ndani ya Jeshi la Polisi kuna nafasi zinazotengwa maalumu kwa kundi fulani la watu?**

Hapana. Hakuna nafasi zinazotengwa maalumu kwa ajili ya kundi fulani la watu katika kuajiri watumishi wa Jeshi la Polisi. Watumishi wa Jeshi la Polisi huandikishwa nchini kote kupitia ofisi za mikoa kwa kuzingatia sifa. Aidha

kuna nafasi zinazotengwa kimkoa na kijinsia ili kuweza kuwapata wanawake wanaoweza kujiunga na Jeshi la Polisi lakini siyo lazima wazawa wa mkoa husika ndio wapate nafasi hata kama hawana sifa.

**16. Je, kuna ulazima gani wa kuajiri wanawake, waislamu, wakristo, makabila mbalimbali na makundi mengine ndani ya Jeshi la Polisi?**

Ni muhimu Jeshi la Polisi kuwa na mchanganyiko wa wanaume na wanawake na watu kutoka dini zote, makundi mbalimbali, na makabila yote. Hii inasaidia kuongeza uelewa wa tabia na mtazamo wa jamii mbalimbali na tamaduni zao na inasaidia kuondoa fikra potofu. Pia inawasaidia wanawake kujiamini na kuonesha uwezo wao katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ambayo awali yalionekana kuwa ni ya wanaume.

**17. Je, nitamtambuaje kuwa mtu huyu ni afisa wa polisi na siyo afisa mwingine tofauti na polisi?**

Askari polisi ana sare za kipekee za rangi ya khaki au bluu na chepeo, mkanda wenye rangi za bendera ya taifa, na alama ya mabegani inayoonesha cheo chake na kitengo au idara aliko na kofia yenye nembo ya taifa, polisi wa usalama barabarani wana sare nyeupe za khaki kwa wanaume na kofia nyeupe na kwa wanawake wana mashati meupe, sketi za bluu na kofia nyeupe. Askari polisi lazima pia wawe na kibandiko kifuani kinachooonesha namba ambayo ni tofauti na askari wegine wasio polisi.

**18. Vyeo vya Jeshi la Polisi ni vipi?**

Jeshi la Polisi Tanzania lina jumla ya vyeo 15 ambavyo ni:

(i) Inspekta Jenerali wa Polisi
(Inspector General of Police - IGP)

(ii) Kamishna wa Polisi
(Commissioner of Police - CP)

(iii) Naibu Kamishna wa Polisi
(Deputy Commissioner of Police - DCP)

(iv) Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi
(Senior Assistant Commissioner of Police - SACP)

(v) Kamishna Msaidizi wa Polisi
(Assistant Commissioner of Police - ACP)

(vi) Mrakibu Mwandamizi wa Polisi
(Senior Superintendent of Police -SSP)

(vii) Mrakibu wa Polisi
(Superintendent of Police - SP)

(viii) Mrakibu Msaidizi wa Polisi
(Assistant Superintendent of Police - ASP)

(ix) Mkaguzi wa Polisi (Inspector of Police - INSP)

(x) Mkaguzi Msaidizi wa Polisi (Assistant Inspector of Police - A/INSP)

(xi) Mnadhimu wa Kambi (Regimental Sergeant Major - RSM)

(xii) Stesheni Taji (Station Sergeant - SSGT)

(xiii) Sajenti (Sergeant - SGT)

(xiv) Koplo (Corporal)

(xv) Konstebo wa Polisi (Police Constable - PC)

### 19. Je, polisi wanaruhusiwa kutumia nguvu?

Katika mazingira ya kawaida askari polisi haruhusiwi kutumia nguvu dhidi ya mtuhumiwa yeyote isipokuwa tu kama mtu huyo anakataa kukamatwa au anajaribu kutoroka. Ijapokuwa askari polisi anaweza kutumia nguvu, lakini hayuko juu ya sheria, na iwapo atatumia nguvu isivyohitajika atachukuliwa hatua za kinidhamu au kufunguliwa mashtaka kwa kosa la jinai.

### 20. Kila polisi anafanya kazi yoyote ndani ya jeshi hilo?

Hapana. Kila askari polisi kutoka ngazi ya konstebo mpaka IGP hupangiwa kazi maalumu. Kazi hizi zimeorodheshwa kwenye kanuni za Kudumu za Polisi (Police General Orders). Askari polisi mwenye cheo cha chini hawezi kufanya kazi alizopangiwa askari polisi mwenye cheo cha juu. Kwa mfano konstebo wa polisi hawezi kufanya kazi alizopangiwa koplo. Hata hivyo, chochote kinachoweza kufanywa na askari polisi wa cheo cha chini kinaweza kufanywa na askari polisi wa cheo cha juu pia.

### 21. Je askari polisi wa usalama barabarani anaweza kunikamata kwa kosa lisilohusiana na usalama barabarani?

Ndiyo. Kimsingi polisi wa usalama barabarani pia ni polisi wa kawaida, aliyepewa majukumu ya usalama barabarani. Akikuona unafanya uhalifu wowote anaweza kukukamata kama polisi mwingine yeyote anavyoweza kukukamata au kama mwananchi yeyote anavyoweza kufanya hivyo ili kuzuia uhalifu. Kama raia akimkamata mhalifu analazimika kumpeleka kwa askari polisi aliye karibu au kituo cha polisi kilichopo karibu mara moja.

### 22. CID ni nini?

CID inamaanisha idara ya upelelezi wa makosa ya jinai. Kwa lugha ya Kiingereza ni “Criminal Investigation Department.” Muda mwingine inaitwa

idara ya upelelezi. Ni idara ya upelelezi ya Jeshi la Polisi. Maafisa katika idara hii wanapaswa kupeleleza makosa makubwa kama vile: ulaghai, udanganyifu, wizi, unyang'anyi wakutumia silaha, ugaidi, uhujumu uchumi na uhalifu ambao unaathari kwa taifa na mataifa.

**23. Kuna utofauti gani kati ya CID na polisi wa kawaida?**

Hakuna tofauti yoyote. Maafisa wa upelelezi wanachaguliwa kati ya askari polisi wa kawaida ambao wamefanya kazi za kawaida za jeshi hilo kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi.

**24. Nani mkuu wa Jeshi la Polisi?**

Kuna Inspekta Jenerali wa Polisi au kwa kifupi 'IGP' mmoja tu nchini anayesaidiwa na makamishna wa polisi pamoja na wakuu wa polisi wa mikoa. Hiki ni cheo cha juu kabisa katika Jeshi la Polisi. Lakini hata yeye Inspekta Jenerali wa Polisi anapaswa kuwajibika Serikalini.

**25. Kwa nini Inspekta Jenerali wa polisi awajibike kwa Waziri?**

Kila serikali duniani inawajibu wa kuhakikisha kuwa kila mmoja wetu anakuwa huru na salama na hana wasiwasi juu ya maisha yake na mpendwa wake au mali yake. Serikali inatoa jukumu hili kwa polisi. Hivyo, polisi wanatakiwa kutoa taarifa serikalini kuhusu jinsi inavyotekeleza kazi zao. Vivyo hivyo, serikali pia inawajibu kwa umma kuhakikisha kuwa polisi ni wakweli, wanatenda haki, na wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi kulingana na sheria na siyo kwa matakwa yao.

**26. Je, ni nani anayetoa fedha kwa ajili ya shughuli za kipolisi?**

Polisi wanalipwa na walipa kodi ili kutoa huduma. Mishahara yao inatoka kwenye bajeti ya serikali kuu. Lakini, mwisho wa yote hayo inatoka mifukoni mwa walipa kodi.

**27. Je, Jeshi la Polisi linapata wapi fedha zake?**

Nchi ina bajeti ambayo hutengwa kwa ajili ya utoaji wa huduma za polisi katika jamii. Jeshi la polisi hupata fedha kutoka kwenye bajeti hii na kutoka kwa wadau wa ndani na wa nje wa maendeleo ya nchi na ya Jeshi la polisi.

**28. Nani hupitisha bajeti na kiasi kikubwa cha bajeti hiyo kinatumika kwa shughuli ipi?**

Bajeti inapitishwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa sababu ulinzi na usalama ni suala la Muungano. Rasimu ya kwanza ya bajeti hiyo inaandaliwa na kitengo cha mipango cha Jeshi la Polisi. Rasimu hii




hupelekwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa ajili ya kuridhiwa. Kutoka hapo hupelekwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tayari kwa kupelekwa bungeni. Baada ya kujadiliwa bungeni, hatimaye bajeti ya polisi ya mwaka hupitishwa. Sehemu kubwa ya bajeti hii hutumiwa kulipa mishahara. Maeneo mengine ya matumizi ni mafunzo, upelelezi, miundombinu, ujenzi wa nyumba n.k.

**29. Je, tunajuaje kuwa fedha wanazo pata Polisi zina tumika vizuri?**

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hufanya ukaguzi wa akaunti na fedha zilizotumiwa na jeshi la polisi kila mwaka. Taarifa za ukaguzi huu huwasilishwa bungeni. Baada ya uchunguzi taarifa hizi pia hupatikana ndani ya Jeshi la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na katika maktaba ya Bunge. Kwa kuwa kazi 14 za polisi zinafanywa kwa kutumia fedha za walipa kodi ambazo ni fedha zako, unawajibika kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa kazi za polisi zinatumika ipasavyo.

## 30. Je, Jeshi la Polisi linaongozwa na sheria gani?

Jeshi la Polisi linaongozwa na Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya 1977, Sheria ya Jeshi la Polisi na Wasaidizi wa Polisi (Sura ya 322 ya Sheria za Tanzania), ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mara kwa mara, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Kanuni za Polisi (Police General Orders).

## 31. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Ushahidi na Kanuni za Adhabu, ni nini?

**Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai** inaeleza njia ambazo polisi na mahakama wanapaswa kufuata katika kuwashughulikia wahalifu. Hii ni pamoja na mamlaka ya polisi na taratibu wanazotakiwa polisi wazifuate. Kwa mfano, kitendo kimojawapo kinaelezea matumizi ya nguvu ya polisi pale anapomkamata mtuhumiwa na sehemu nyingine inaelezea nguvu na kazi za polisi anapofanya uchunguzi.

**Sheria ya Ushahidi** inaeleza kwa undani kinachokubalika mahakamani kama ushahidi. Kwa mfano, sehemu moja ya sheria hiyo inasema kuwa ushahidi uliopatikana kwa kutumia nguvu hauwezi kutumika kama ushahidi halali, kama ikibainika na mahakama kuwa ulipatikana kwa njia zisizo halali.

**Kanuni ya adhabu (Penal Code)** inatoa ufafanuzi wa kila uhalifu unaosadikiwa kuwa ni matendo ya kihalifu nchini Tanzania. Pia inaelezea tabia na matendo, yanayoitwa makosa, yanafuatiwa na adhabu kwa kila kosa.

## 32. Sheria ya Polisi inasemaje?

Sheria ya polisi kwa kawaida inaeleza kuhusu uendeshaji wake, nidhamu, mamlaka na kazi za Polisi, Polisi wa Akiba na Polisi wasaidizi na mambo mengine yanayolihusu jeshi hilo. Inaeleza kwa kina njia mbalimbali zinazopaswa kuchukuliwa katika kuhakikisha haki na utendaji wa kulinda sheria na kanuni za nchi zinafanyika kwa haki na kwa uwazi.

## 33. Nini maana ya "Utawala wa Sheria"?

Hii ina maana kuwa sisi, sote, mkubwa au mdogo, tajiri au maskini, mwanaume au mwanamke, hata serikali na watumishi wa umma kama vile polisi, tunatakiwa kutii sheria na lazima tuishi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa nchini mwetu chini ya Katiba yetu. Hakuna aliye juu ya sheria. Pia ina maana kuwa kila tendo linalofanywa na askari polisi lifanywe kulingana na sheria, na iwapo hatafanya hivyo askari polisi huyo atawajibika mbele ya sheria. Vilevile inamaanisha kuwa sheria zinazotungwa ni lazima ziwe za haki na usawa.

**34. Je, polisi anaweza kumkamata polisi mwenzake kwa tuhuma za rushwa?**



Ndiyo. Jina zuri la Jeshi la Polisi na sifa njema ya watumishi wake inategemea sana uadilifu na uaminifu wa kila polisi. Kila tendo la rushwa au tuhuma za rushwa dhidi ya askari polisi katika utekelezaji wa shughuli zake inatoa sifa mbaya kwa Jeshi la Polisi. Hivyo, kila polisi anayefahamu kuwa polisi mwenzake anajihusisha na vitendo vya rushwa halafu akashindwa kuchukua hatua yoyote ile atakuwa anafanya makosa. Wote waliopo kwenye mamlaka ambao watashindwa kutoa taarifa ya kuwepo au kuhisi dalili za rushwa wanajiweka kwenye nafasi ya kuhisiwa kushiriki.

Mwananchi na polisi anayehisi au kuwa na taarifa ya rushwa lazima atoe taarifa kwa Kamanda wa Polisi wa Wilaya au afisa wa polisi mwenye cheo cha Mrakibu Msaidizi na kuendelea na wakuu wa vituo vya polisi.

**35. Askari polisi anaweza kuadhibiwa akifanya makosa?**

Ndiyo. Askari polisi kama mtu mwingine yeyote iwapo atavunja sheria anaweza kuadhibiwa. Kwa kweli kwa kuwa yeye ni mtu aliyepewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria anatakiwa kupewa adhabu kali zaidi kwa kuvunja sheria.

**36. Askari polisi anaadhibiwaje?**

Kuna njia nyingi za kuwaadhibu askari polisi waliofanya makosa. Kama ametenda kosa la jinai hivyo anaweza kupelekwa mbele ya mahakama na akahukumiwa kama mtu mwingine yeyote au akapelekwa mahakama ya kijeshi kutegemeana na ukubwa wa kosa linalomkabili. Iwapo amekosa adabu, amekuwa na tabia mbaya au hakutekeleza majukumu yake inavyotakiwa, ataadhibiwa kulingana na taratibu na kanuni za Jeshi hilo.

**37. Askari polisi wanafanyakazi hatarishi. Je, wanakinga ya bima?**

Hapana, askari polisi wa Tanzania hawana bima. Familia ya askari polisi aliyeuwawa au kufariki kazini inapewa fidia na yule aliyeumia kazini anaweza akalipwa fidia au posho kulingana na matakwa ya waziri mwenye dhamana.

**38. Je, askari polisi anatakiwa kukubali kila amri aliyopewa na mkuu wake wa kazi au mtu yeyote mwenye mamlaka ya kutoa amri kama vile Waziri, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Makamishna mbalimbali n.k?**

Hapana. Askari polisi lazima atii amri ikiwa tu ni halali. Anaweza akawajibika kwa chochote kibaya atakachokifanya kama ameamriwa kufanya hivyo. Kamwe hawezi kujitetea kwa kusema kuwa mkuu wake au mtu fulani mwenye mamlaka alimwamuru kutenda jambo baya na lililo kinyume cha sheria. Hilo halitamlinda.

**39. Je, askari polisi yuko kazini muda wote?**

Ndiyo. Kulingana na kanuni za Polisi kama zilivyorekebishwa Mwaka 2006 ipo wazi kuwa askari polisi muda wote yupo kazini. Lakini hiyo haina maana kuwa haruhusiwi kupumzika. Hii ina maana kuwa popote alipo, akivaa au kuvua sare zake, lazima ajihusishe kulinda sheria. Hawezi kusema "sipo kazini" kama anashuhudia uhalifu unatendeka au anasikia mtu anaomba msaada.

**40. Je, naweza kupewa polisi kwa ajili ya ulinzi wangu binafsi?**

Unaweza iwapo askari polisi atakuwa na kibali cha Inspekta Jenerali Mkuu wa polisi. Sheria inasema,"Inspekta Jenerali Mkuu anaweza, kutokana na maelekezo ya Waziri, katika maombi ya mtu yeyote na baada ya kuridhika kutokana na umuhimu wa ombi hilo, kutoa namba yoyote ya maafisa polisi kwa ajili ya kazi maalum katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano kwa kipindi ambacho kinaweza kuzingatiwa kuwa ni lazima. Maafisa polisi hao, kulingana na masharti ya Sheria hii, watakuwa chini ya amri ya afisa mwandamizi wa polisi katika sehemu hiyo na, isipokuwa Waziri ameelekeza vinginevyo, wataajiriwa kwa gharama za mtu aliyefanya maombi."[1] Hakuna askari yeyote wa polisi, bila ya kibali cha Inspekta Jenerali Mkuu, atajihusisha na ajira nyingine yoyote ile au ofisi kwa namna yoyote ile isipokuwa kwa kufuatia wajibu wake chini ya Sheria ya polisi.

**41. Je, askari polisi wanayo ruhusa ya kupata huduma bure?**

Sehemu nyingine askari polisi wanapewa pasi ya kusafiria katika usafiri wa umma pale wanapokuwa kazini tu. Lakini hakuna askari polisi anayeruhusiwa kusafiri bure katika usafiri wa umma. Vivyo hivyo sokoni; hakuna askari polisi anayeweza kuchukua mahitaji kutoka sokoni kwa ajili ya kulipa baadaye kwa sababu tu yeye ni askari polisi. Kama vile walivyo wananchi wengine anapaswa kulipia mahitaji anayoyachukua.

**42. Je, natakiwa kuzingatia kila agizo la askari polisi?**

Ndiyo, kama ni amri halali inayohusiana na kazi yake. Kiukweli kila mmoja ana wajibu wa kumsaidia askari polisi katika kutekeleza kazi yake; hasa iwapo polisi anajaribu kusimamisha mapigano au kuzuia uhalifu au anajaribu kumzuia mtu kutoroka katika ulinzi wake. Ki ukweli, iwapo unazo taarifa zinazohusu uhalifu ni wajibu wako kupeleka taarifa hizo kwa polisi. Pia ni wajibu wako kutomhifadhi mtu anayejulikana kuwa ni mhalifu. Vilevile una wajibu wa kutoa ushahidi mahakamani endapo unajua au umeona kitu fulani kuhusiana na shauri lililoko mahakamani.

**43. Je, naweza kuambatana na askari polisi iwapo ataniomba kufuatana naye mahali fulani?**

Hapana. Hata hivyo, iwapo askari polisi anakuomba ufuatane naye ili ukawe shahidi wa kitu anachokifanya kama sehemu ya kazi yake, kama vile kumkamata mtu, kutwaa mali, au kuchunguza eneo la uhalifu, hivyo unaweza kuambatana naye na kumsaidia. Kwa kawaida mtu huyo anaitwa shahidi anayeweza kuieleza mahakama alichokiona bila kuegemea upande wowote.

Katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, watu walioko chini ya “kizuizi” – watu ambao hawakukamatwa na askari polisi, lakini askari polisi asingependa kuwaruhusu waondoke kwa vile wanaweza kuwa na taarifa kuhusiana na uhalifu – wanaweza kushikiliwa kwa ajili ya kuhojiwa na polisi ndani ya masaa manne (4) tangu walipowekwa chini ya kizuizi. Ikiwa uko chini ya kizuizi unayo haki ya kuongea na mwanasheria au ndugu au rafiki.

**44. Ikitokea askari polisi ananiomba kwenda kituoni, je naweza kwenda?**

Hapana. Ni vizuri kushirikiana na polisi lakini siyo muhimu kwenda kituo cha polisi isipokuwa kama askari polisi amekukamata rasmi kwa utaratibu unaotambuliwa. Vinginevyo, iwapo anataka kukuhoji au anafanya uchunguzi kuhusu uhalifu, anatakiwa kukuletea wito wa maandishi wa kukutaka ufike kituoni. Mpaka hilo lifanyike huwezi kulazimishwa kwenda kituoni.

**45. Je, ni lazima nijibu maswali yote anayouliza askari polisi?**

Ni vizuri kujibu maswali yote kwa ukweli na uwazi na kuwaeleza askari polisi mambo yote yaliyotendeka unayoyajua kuhusiana na tukio husika. Iwapo hujui chochote, askari polisi hawezi kukulazimisha kutoa maelezo au kukusemea. Daima ni vizuri kuhakikisha kuwa mtu mwingine yuko pamoja nawe wakati unapohojiwa.




Pia, iwapo askari polisi anaamini kuwa unaweza kusaidia katika upelelezi wa uhalifu, anaweza kukuomba umpe jina lako na anuani yako. Ni lazima umweleze kila kitu, hata hivyo unaweza pia kumwomba askari huyo kukupatia jina lake, cheo chake na kituo chake cha kazi. Askari polisi anatakiwa kutekeleza hili akiombwa.

**46. Je, askari polisi anawajibu wa kunisadia wakati wa dharura?**

Ndiyo. Askari polisi anatakiwa kutoa msaada kwa kila mtu bila kujali utajiri na hali ya kimaisha ya mtu, au nafasi ya mtu katika jamii. Kulingana na

kanuni za maadili kazi kubwa ya polisi ni kutoa ulinzi kwa kila mtu bila woga au upendeleo ikiwa ni pamoja na kuwatuliza watu kiakili, kuhuzunika nao na kuwajali, kuwa tayari kutoa huduma na kuwa na uhusiano nao.

### 47. Je, naweza kumwomba askari polisi kunisaidia katika matatizo ya kifamilia?

Inategemea na aina ya tatizo. Iwapo kinachotokea ni uhalifu kama wa kufanya vurugu katika familia, kumpiga vibaya mwanamke au mtoto, au wanandugu kujamiiana, kuvamia eneo la mtu mwingine, bila shaka polisi lazima akusaidie hawezi kukuachia na kusema kuwa hilo ni suala lako binafsi. Lakini iwapo watoto wako wakubwa (wenye umri wa miaka 18 au zaidi) ni wakaidi, tuseme wanatoroka nyumbani na kwenda kuolewa, hiyo siyo kazi ya polisi kuwafuatilia au kuwalazimisha warudi nyumbani. Kabisa hilo ni suala la kifamilia; isipokuwa kama watoto hao wapo chini ya umri wa miaka 18.

### 48. Iwapo askari polisi hatoi msaada au hayupo karibu, je wananchi wanaweza kumkamata mwizi au mhalifu yeyote na kumwadhibu papo hapo?

Hapana. Unaweza ukafanya kitu kinachoitwa “kuwekwa chini ya ulinzi na wananchi” na kumkamata mhalifu na kumpeleka kituo cha polisi kilichopo karibu. Lakini huwezi kumpiga mhalifu au kushirikiana na kundi la watu wanaofanya hivyo. Wananchi wanayo haki ya kujilinda lakini ulinzi huo uwe kwa kiasi. Haiwezi kugeuzwa kuwa ni kipigo cha upande mmoja au udhalilishaji wa kutisha na askari polisi anayeruhusu hilo au anayeungana na wanaofanya hivyo anaweza kukabiliwa na mashtaka ya kinidhamu au jinai.

### 49. Je, nitafanyaje iwapo askari polisi hataki kunisaidia?

Kuvunjwa kwa makusudi au kudharau wajibu wa kazi kwa askari polisi ni kosa linalostahili adhabu ya kifungo endapo itathibitika. Iwapo askari polisi hana msaada, nawe umedhurika, unaweza kulalamika kuhusu jambo hilo kwa afisa wa polisi wa ngazi ya juu. Katika hali hiyo askari polisi huyo anaweza kuonekana anahatia ya kushindwa kutimiza wajibu wake.

### 50. Je, askari polisi wanaweza kufanya chochote watakacho?

Hata kidogo. Wanaweza kufanya kile tu kinachokubalika kisheria. Kwa kweli wanatawaliwa na kanuni nyingi na kali. Hii ni pamoja na kanuni zao wenyewe, taratibu zilizowekwa kwa ajili ya uhalifu (criminal codes), amri zinazotolewa na mahakama ya rufaa, na miongozo kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

**51. Lakini iwapo askari polisi hawatii sheria hizo inakuwaje?**

Unaweza kulalamika kwa afisa wa polisi wa cheo cha juu yake, au mkuu wa kituo au kwa hakimu au Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kulingana na uzito wa suala lenyewe. Ni vizuri kulalamika kwa maandishi na kupata uthibitisho wa maandishi wa kupokelewa kwa lalamiko lako.

**52. Nitalalamika kuhusu nini hasa?**

Unaweza kulalamika kuhusu tendo lolote ovu ulilotendewa na askari polisi kwa sababu yeye ni mtumishi wa umma anayetakiwa kufanya kazi zake wakati wote kwa uadilifu na uaminifu. Hatakiwi kuzembea katika kazi yake au kuchelewa kuifanya.




**53. Ikitokea askari polisi ni mkorofi na ananitukana nifanyeje?**

Unaweza kulalamika kwa mkuu wake wa kazi kwa kukiuka maadili ya kazi na ukosefu wa nidhamu. Kama ni suala lolote ovu linaloweza kupelekea uhalifu unaweza kufungua jalada la lalamiko dhidi ya askari polisi katika kituo cha polisi au unaweza kwenda moja kwa moja kwenye mahakama ya mwanzo na kufungua jalada la lalamiko lako hapo. Kama huna uhakika ni wapi utapeleka lalamiko lako unaweza kuuliza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora au mwanasheria yeyote aliyekaribu nawe.

**54. Ikitokea nimefungua lalamiko kituo cha polisi, na wakakataa kuchukua hatua dhidi ya askari polisi mwenzao nifanye nini?**

Ndiyo, jambo hili hutokea. Lakini inatakiwa isiwe mwisho wa suala hilo.



Unaweza kupeleka lalamiko kuhusu ufedhuli au utovu wa nidhamu au kuzembea kazi au matumizi mabaya ya mamlaka ya kipolisi kwa mkuu wa polisi au kama ni kosa la jinai unaweza kupeleka kwa hakimu aliye karibu.

### 55. Lakini ni vigumu kupeleka kesi mahakamani kwani inachukua muda mrefu, nitafanyaje?

Ili kurahisisha upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko dhidi ya polisi na kwa kufanya utaratibu uwe rahisi na wa haraka zaidi nchi nyingine wameweka mamlaka zinazopokea malalamiko dhidi ya polisi. Ni mamlaka maalum zinazoshughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya polisi. Kwa hapa Tanzania mamlaka nyingine za kitaifa, nje ya mahakama, ambako mtu yeyote mwenye malalamiko dhidi ya polisi anaweza akapeleka ni pamoja na: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Wizara ya Mambo ya Ndani, na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Mamlaka hizi zitachunguza kwa undani lalamiko lako kulingana na uwezo wao kisheria na wanaweza kulisajili lalamiko dhidi ya polisi.

### 56. Ikiwa nataka kuwapa askari polisi taarifa ya uhalifu, nitafanyaje?

Iwapo ni taarifa ya uhalifu mkubwa kama vile wizi, uvunjwaji wa nyumba, udhalilishaji wa wazi wa kijinsia, shambulio, udhalilishaji wa wazi wa watoto, ubakaji, kumchukua mtu kinguvu na kumshikilia, usafirishaji haramu wa binadamu na fujo unaweza moja kwa moja kufungua jalada lenye taarifa ya awali kwa mkuu wa kituo kidogo na atawajibika kuchukua maelezo na kukupatia nakala ya maelezo husika. Unaweza ukapeleka maelezo ya lalamiko hilo kwa hakimu na atalisajili.

### 57. Taarifa ya awali ni nini?

Ni maelezo ya awali ya tukio lililotokea anayotoa mlalamikaji mbele ya polisi. Mwathirika, shahidi au mtu yeyote anayejua kuhusu uhalifu anaweza kufungua jalada la maelezo ya awali. Unachokieleza kwenye taarifa hiyo ya awali kitasaidia polisi kuanza uchunguzi kuhusu suala hilo na kukusanya ushahidi ili kujiridhisha iwapo kuna kesi inayoweza kufunguliwa au la.

### 58. Nini kinapaswa kuandikwa katika taarifa ya awali?

Taarifa ya Awali ni maelezo ya ukweli kama unaufahamu au kama ulivyoambiwa. Ni vizuri ukiujua ukweli halisi lakini sio lazima kuwepo na kuona uhalifu ukitendeka. Kwa maana hiyo, ni lazima utoe habari sahihi. Usikuze au kukisia au kutoa pendekezo.

Taja sehemu, siku au tarehe na muda wa tukio. Kwa utaratibu eleza wajibu wa kila mtu aliyehusika: walikuwa wapi, walikuwa wanafanya nini, mlolongo wa kila kilichofanyika na kila mtu, kila aina ya majeruhi au uharibifu wa mali

uliofanywa. Usisahau kutaja aina ya silaha iliyotumika. Ni vizuri kuweka kumbukumbu za ukweli na hali halisi haraka iwezekanavyo. Kama kuna kuchelewa katika kuchukua maelezo ya mlalamikaji hakikisha unatoa sababu za kuchelewa.

**59. Nitajuaje kuwa askari polisi ameandika kwa usahihi nilichomwambia?**

Ikumbukwe kuwa Taarifa ya Awali ni maelezo yako ya unachojua. Siyo maelezo ya polisi. Askari polisi yupo pale kunukuu kwa usahihi bila kuongeza au kuondoa kitu chochote. Ili kujiridhisha na hili, sheria inamhitaji askari polisi kukusomea taarifa au kukupa mwenyewe na kuisoma, kufanya marekebisho kwa kuongeza au kupunguza maelezo ya taarifa hiyo ya awali na pindi utakapokubaliana nayo itabidi utie saini. Pia unaweza kuomba uiandike wewe mwenyewe kwa polisi kukupatia vifaa vya kuandikia. Taarifa ya Awali itatunzwa na nakala kupelekwa kwa afisa wa polisi wa cheo cha juu na kwa hakimu.

**60. Je, naweza kwenda kufungua kesi kwenye kituo kidogo cha polisi au katika kituo chochote cha polisi?**

Unaweza kufungua kesi katika kituo chochote cha polisi. Lakini ni vizuri kwenda kwenye kituo kilichopo karibu na uhalifu ulipotendeka kwani watakwenda kwa haraka. Kama utasajili katika kituo chochote cha polisi watasajili lalamiko lako kwa kuwa wanalazimika kufanya hivyo na kupeleka kituo kinachostahili. Hawawezi kukataa kusajili Taarifa ya Awali eti kwa sababu uhalifu haukufanyika katika maeneo ya mamlaka yao.

**61. Je, askari polisi anaweza kukataa kupokea taarifa yangu kuhusu uhalifu?**

Hapana, askari polisi ni lazima asajili taarifa yako kuhusu uhalifu. Hata hivyo, baadhi ya makosa yanahitaji kupata kibali kabla ya askari polisi



kuweza kumkamata mtu, hivyo askari polisi ni lazima kwanza apate kibali kabla ya kumkamata mtu yeyote baada ya kuchunguza ripoti yako.

**62. Iwapo lalamiko langu linahusu kosa la jinai ambalo askari polisi ana uwezo wa kisheria wa kusajili, lakini mkuu wa kituo akakataa kulisajili. Nitafanyaje?**

Unaweza ukasajili lalamiko lako kwa kupeleka lalamiko kwa askari polisi wa cheo cha juu au Mkuu wa polisi (wilaya) au hakimu wa mahakama iliyopo karibu nawe, nao wanaweza kutoa amri ya kusajili lalamiko hilo. Ili kuhakikisha kuwa lalamiko lako linasajiliwa, unaweza kuwasilisha lalamiko lako kwa wewe mwenyewe kwenda kituoni au kulituma kwa njia ya rejesta ya posta. Kwa njia yoyote utakayotumia, hakikisha unapata uthibitisho wa kupokelewa kwa lalamiko lako na mtu aliyepokea. Pia kumbuka kulalamika kuhusu ugumu wowote ulioupata katika kusajili lalamiko hilo ili kuhakikisha kuwa askari polisi aliyesababisha ugumu huo haendelei tena na tabia hiyo.

**63. Kinaendelea nini baada ya kufungua jalada la taarifa yangu ya awali?**

Taarifa ya awali inawasaidia polisi kupanga na kuanzisha uchunguzi. Katika uchunguzi huo polisi wanaweza kuongea na waathirika na mashahidi, kuchukua maelezo ikiwa ni pamoja na maelezo ya mtu mwenye akili timamu na anayekaribia kufa baada ya tukio fulani, kuchunguza eneo la uhalifu, kuchunguza maiti, kupeleka sampuli kwa uchunguzi wa kimaabara na kufanya uchunguzi mwingine wa kina.

**64. Je, ni kitu gani kinaendelea uchunguzi wote unapokuwa umekamilika?**

Baada ya uchunguzi wote kuwa umekamilika askari polisi aliye na madaraka atayaangalia maelezo yaliyotolewa na kuamua iwapo kuna ushahidi wa kutosha wa kuonesha kuwa uhalifu ulitendeka na kumfungulia mashtaka ya jinai mtu aliyehusika. Polisi ataandaa taarifa ya mwisho kwa ajili ya mwendesha mashtaka, ambayo kwa maoni ya afisa wa upelelezi inaonesha kuwa kuna ushahidi na taarifa za kutosha kwa mahakama kulisikiliza shauri. Hivyo mtuhumiwa atashtakiwa mbele ya mahakama kwa uhalifu na itaonekana kama hana hatia au mhalifu.

**65. Je, askari polisi atamkamata kila mmoja aliyetajwa ndani ya taarifa ya awali?**

Hapana, kama umetajwa kama shahidi hawatakiwi kufanya hivyo. Mtu kutajwa katika taarifa ya awali siyo sababu inayojitosheleza ya kukamatwa kwake. Ni pale tu kutakapokuwa na sababu za kutosha za kuonyesha kuwa

mtu huyo amehusika katika kufanya uhalifu ndipo askari polisi wanaweza kumkamata.

**66. Je, askari polisi anaweza kulifunga lalamiko langu bila kuchukua hatua zaidi?**

Ndiyo. Polisi wanaweza kuamua kufunga shtaka baada ya kutoa sababu za kufikia uamuzi huo mahakamani iwapo baada ya kufanya uchunguzi wao hawakuweza kupata ukweli unaosaidia kuonyesha kuwa uhalifu ulitendeka au iwapo hakuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kuwa kuna ukweli katika tuhuma zilizotolewa au kuthibitisha kuwa uhalifu umefanyika lakini watu waliofanya uhalifu huo hawajulikani. Hata hivyo, sharti wakufahamishe juu ya uamuzi wao. Nawe unayo nafasi ya kupinga kufungwa kwa lalamiko lako mbele ya mahakama.

**67. Je, naweza kuendelea kupewa taarifa ya maendeleo ya kesi yangu?**

Hakuna kipengele maalumu katika sheria kinachomtaka askari polisi kukufahamisha kuhusu maendeleo ya kesi yako. Lakini ni utendaji mzuri kumweleza mlalamikaji mwenendo wa kesi yake iwapo kufanya hivyo hakutaathiri upelelezi. Hata hivyo, hilo litawezekana tu iwapo kesi hiyo itakuwa bado ipo chini ya usimamizi wa polisi, lakini ikiwa kwa mwendesha mashtaka wa serikali itakuwa vigumu kwa polisi kukupatia maendeleo hayo.

**68. Nifanye nini iwapo askari polisi hawalichunguzi jambo langu au wanafanya pole pole au wanakataa kuchunguza masuala yaliyowazi katika mkondo wa uchunguzi?**

Kuna kanuni muhimu katika Sheria kuwa hakuna mtu awezaye kuingilia upelelezi wa polisi. Hivyo iwapo polisi wanakataa kuendelea na upelelezi au wanafanya hivyo pole pole sana au kwa makusudi wakapuuza masuala



muhimu katika mkondo wa upelelezi hakika unaweza kulalamika kwa askari polisi wa cheo cha juu au kwa hakimu aliye jirani ambaye atamwamuru askari polisi huyo kupeleleza suala hilo na pia anaweza akahitaji apewe taarifa ya upelelezi huo. Pia ni muhimu ukahakikisha kuwa kila kitu kinafanywa kwa maandishi na unatunza kumbukumbu za kupokelewa kwa nyaraka zako.

### 69. Je, naweza kumwita askari polisi wakati wowote ninapohitaji?

Ndiyo na hapana. Polisi wanafanyakazi nyingi na wako wachache, hivyo wananchi hawatakiwi kila wakati kuwaita kwa malalamiko yasiyo ya msingi na taarifa zisizothibitishwa. Hata hivyo, unaweza kuwaita polisi iwapo uko matatani, kuna uhalifu umetokea au unatokea, au kuna uwezekano wa kutokea ghasia, watu wanapigana na kuna uwezekano wa kutokea machafuko, au iwapo una taarifa nzito ya kuwapatia. Lakini huwezi kuwaita polisi kwa suala lisilohusiana na kazi yao. Wakati mwingine watu wanafanya utani na wanawaita polisi hata kama hakuna jambo lolote lililotokea. Unaweza kuadhibiwa kwa mzaha huo.

### 70. Hati ya upekuzi ni nini?

Ni hati inayotolewa na hakimu ambayo inampa askari polisi ruhusa ya kupekua sehemu yenye uwezekano wa kuwepo ushahidi unaohusiana na kosa lililofanyika au ushahidi kuhusu kosa linalodhaniwa kuwa litatendeka. Nyumba na ofisi za watu ni maeneo ya faragha na hayawezi kuwa huru kwa mamlaka yoyote kuingia na kupekua bila ya sababu za msingi. Hivyo Sheria inamtaka yeyote anayehitaji kuingia katika maeneo binafsi kueleza kwa nini anaona kuwa ni muhimu kuingilia haki ya mtu ya faragha.




### 71. Je, polisi wanapataje hati ya upekuzi?

Askari polisi wanatakiwa waende mbele ya hakimu na kueleza sababu zinazowafanya wafikiri kuwa kuna mali, nyaraka au watu waliofichwa kwenye nyumba husika ambapo kukamatwa kwao kutasaidia kuleta suluhisho la uhalifu. Iwapo hakimu atashawishika kuwa kuna sababu za msingi za kufanya upekuzi wa majengo hayo, atatoa kibali. Kibali hicho kina mipaka na kinatoa jina na cheo cha askari polisi anayeruhusiwa kuingia ndani ya jengo husika na kinatolewa chini ya saini na muhuri wa moto wa mahakama.

Mkuu wa kituo cha polisi pia anaweza kutoa hati ya upekuzi kwa sababu zilizotajwa hapo juu, lakini atafanya hivyo tu iwapo ataridhika kuwa ucheleweshaji wowote utakaotokana na kuomba kibali cha upekuzi kwa

hakimu kutasababisha kuondolewa au kuharibiwa kwa ushahidi, au kutahatarisha uhai au mali. Askari polisi lazima pia atoe taarifa ya utolewaji wa hati ya upekuzi kwa hakimu aliyepo eneo la karibu, akieleza kwa nini alitoa hati ya upekuzi na mali zilizoonekana kutokana na upekuzi uliofanyika.

Askari polisi wanaweza kusimamisha na kupekua gari iwapo wataamini kuwa ndani yake kuna mali za wizi, vitu vilivyotumika au vitakavyotumika katika uhalifu, au silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria. Hii ni tofauti na kupekua nyumba.

**72. Je, askari polisi anaweza kuingia ndani ya nyumba yangu bila kukaribishwa, kuipekua na kuchukua kitu chochote?**

Inawezekana katika mazingira machache sana. Iwapo askari polisi watakuja nyumbani kwako kwa mahojiano wataweza kuingia ndani pale tu utakapowakaribisha. Hata hivyo, hata kama askari polisi wanasababu za msingi za kuamini kuwa unamficha mtuhumiwa au wahalifu au una mali ya wizi au nyumbani mwako kuna silaha inayomilikiwa isivyo halali, wataweza tu kuingia nyumbani mwako wakiwa na hati ya upekuzi kutoka kwa mkuu wao wa kazi au hakimu. Lakini ikiwa mtuhumiwa, mhalifu au kitu kinatakiwa kipatikane bila kuchelewa na kuna hofu kitapotea iwapo hakitatwaliwa wakati huo basi wanaweza kuingia nyumbani mwako bila hati ya upekuzi.

**73. Una maana kuwa askari polisi anaweza kuingia ndani ya nyumba yangu na kuchukua kitu chochote na kuondoka nacho?**

Hapana. Inawezekana tu iwapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo – kwa mfano iwapo kweli kuna uwezekano wa mtuhumiwa kukimbia na askari



polisi anazo sababu zinazomfanya aamini hivyo au iwapo kuna uwezekano wa ushahidi kuharibika, hivyo askari polisi anaweza kuingia ndani ya nyumba yako bila hati ya upekuzi. Na ikiwa askari polisi atachukua kitu chochote ndani ya nyumba lazima atoe risiti ya kukubali kukamata mali hizo, ikiwa na saini ya mmiliki, au mkazi wa makazi hayo au ndugu yake wa karibu na saini ya mashahidi walioshuhudia upekuzi huo, kama wapo.

Hati ya upekuzi iwepo au isiwepo bado kuna utaratibu unaotakiwa kufuatwa. Upekuzi lazima ufanyike mmiliki akiwepo. Mmiliki hatakiwi kuondolewa wakati upekuzi unaendelea. Polisi wanatakiwa kuorodhesha vitu wanavyovichukua. Mashahidi, askari polisi na mmiliki wa nyumba au ofisi lazima watie saini kuthibitisha vitu vilivyochukuliwa. Lazima nakala iliyosainiwa na wote iachwe kwa mmiliki. Iwapo ndani ya nyumba kuna mwanamke, ambaye hatakiwi kukamatwa, na ambaye kwa mujibu wa mila hatakiwi kutoka nje, askari polisi anatakiwa atoe taarifa kwa mwanamke huyo ya kumtaka aondoke ndani ya nyumba hiyo na atoe muda wa kutosha wa mwanamke huyo kuondoka.

Iwapo wanawake wanatakiwa kupekuliwa, upekuzi huo lazima ufanyike na askari wa kike kwa uangalifu na heshima ya hali ya juu.

Upekuzi lazima ufanywe kati ya kuchomoza na kuzama kwa jua, isipokuwa iwapo mahakama imeamuru vinginevyo.

### 74. Nikiwa natembea mtaani, je askari polisi anaweza kunisimamisha na kuniuliza chochote anachopenda?

Hapana. Kwa ujumla askari polisi hawatakiwi kuwaingilia watu wanaofanya shughuli zao halali. Lakini iwapo atakudhania kuwa unazurura mtaani hususan wakati wa usiku anayo haki ya kukusimamisha na kukuuliza jina lako na shughuli unayofanya. Ikiwa kuna kitu anachokitilia shaka juu ya jambo fulani unaweza kukamatwa. Askari polisi wanatumia mamlaka haya mara nyingi kama njia ya kuwakamata washukiwa na watu wenye mazoea ya kufanya uhalifu. Aidha, matumizi yaliyovuka mpaka ya mamlaka haya yamejadiliwa mara nyingi na kamati za maboresho na kulaaniwa.

### 75. Je, askari polisi anaweza kunizuia nisishiriki kwenye maandamano au mkutano wa hadhara?

Unayo haki ya kushiriki katika maandamano ya amani. Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki kwa kila mtanzania kushiriki katika mikusanyiko ya amani. Lakini taarifa ya maandishi lazima itolewe polisi saa 48 kabla ya kufanyika kwa mkusanyiko au maandamano katika maeneo ya wazi. Taarifa hiyo lazima itolewe kwa kiongozi wa polisi wa eneo ambako mkusanyiko huo unapendekezwa kufanyika. Askari polisi

anayepokea taarifa hiyo anaweza kusema kuwa mkutano unaopendekezwa hauwezi kufanyika iwapo anaamini kuwa mkutano huo unaweza kusababisha uvunjifu wa amani, usalama wa umma, kudumishwa kwa utulivu, kutumiwa kwa makusudi yaliyo kinyume cha sheria au iwapo matakwa ya utoaji wa taarifa ulioelezwa hapo juu haukutimizwa.

Iwapo yanafanyika na baadaye yakageuka machafuko, polisi wanaweza kuyazuia yasiendelee, wakawataka wananchi waondoke na kuchukua hatua iwapo hawatawanyiki.

Kwa upande mmoja askari polisi wana wajibu wa kuhakikisha kuwa amani inakuwepo. Kwa upande mwingine, askari polisi wana wajibu wa kuwawezesha wananchi kutumia haki yao ya msingi ya kufanya mikutano ya hadhara kwa amani na utulivu.

### 76. Je, polisi wanaweza kutumia nguvu kuvunja mkutano wa mtaa au maandamano?

Ndiyo. Chochote polisi wakifanyacho kinatakiwa kuwa kwa kiasi. Hawapo kwa ajili ya kuwaadhibu watu, wapo pale kuhakikisha watu wapo salama na sheria na amani hazivunjwi. Hivyo kanuni ni kwamba katika kudhibiti mkusanyiko wa watu askari polisi watatumia nguvu kama suluhisho la mwisho baada ya hatua nyingine zote kushindikana. Kama nguvu italazimika kutumika basi iwe ya kadiri, inayoendana na mazingira na itumiwe kwa muda mfupi iwezekanavyo.

### 77. Je, askari polisi anaweza kutumia bunduki (nguvu kubwa inayoweza kusababisha maangamizi?)

Nguvu kubwa zitumike inapolazimika tu, wakati njia nyingine zote za udhibiti zikiwa zimejaribiwa na kushindikana. Askari polisi anaweza kutumia bunduki dhidi ya mtu anayetoroka, au anayefanya jaribio la kutoroka toka kizuizini au kutoroka asikamatwe - lakini pale tu askari polisi anapokuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hawezi kuzuia utoro huo kwa njia nyingine na ametoa onyo kwa mtu huyo kuwa yuko karibu kutumia bunduki, na mtu huyo hajali onyo lililotolewa.

Pia askari polisi anaweza kutumia bunduki dhidi ya mtu ambaye anatumia nguvu kumwondoa mtu mwingine kutoka kizuizi halali au kuzuia ukamatwaji halali wa mtu mwingine. Hata hivyo, katika suala hili, askari polisi anaweza tu kutumia bunduki iwapo hakuna njia nyingine ya kumzuia mtu huyo na iwapo askari polisi ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtu mwingine, au askari polisi wenyewe, wako hatarini kuumizwa vibaya.




**78. Je, askari polisi afanye nini kama watu ni wakaidi na wanarusha mawe au kuharibu mali?**

Askari polisi wana wajibu wa kulinda uhai na mali za watu. Lakini kuna utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa jukumu hilo. Kwanza kutoa onyo mara tatu la kuwataka watu watawanyike na muda wa kutii amri hiyo lazima utolewe. Kama bado hawatawanyiki nguvu ya kadiri inaweza kutumika. Na aina ya nguvu hizo ni matumizi ya mikanda ya ngozi, virungu au silaha zinaweza kutumika pia kama vile risasi za mpira, maji ya kuwasha au mabomu ya machozi. Virungu visipigwe kichwani na mabegani bali vilengwe chini ya kiuno. Wakati wote polisi lazima wajitahidi kutumia njia yenye madhara kidogo na kutumia njia nyingine kama ile imeshindikana. Iwapo polisi watatumia risasi za moto wafanye hivyo kama njia ya kujihami, na lazima pawepo na maonyo ya wazi kuwa risasi zitatumika. Hapa pia kanuni ni kutumia nguvu kiasi. Hivyo, upigwaji wa risasi lazima ulenge chini na katika sehemu ya kundi inayoonekana kuwa tishio siyo kwa lengo la kusababisha mauaji bali kuwatawanya. Mara kundi hilo linapoonyesha dalili ya kutawanyika upigaji wa risasi lazima usimamishwe. Majeruhi lazima wasaidiwe kwa kupelekwa hospitali mara moja. Hata hivyo kila askari polisi anawajibika kuandika taarifa ya uhusika wake kwa ajili ya kumbukumbu. Lakini njia iliyobora ni ile ya kushauriana kwa mazungumzo na waandamanaji.

**79. Je, askari polisi wanaweza kunishikilia mafichoni au wasimweleze mtu yeyote kuwa wananishikilia?**

Hapana. Baadhi ya askari polisi wamezoea kufanya hivyo mara kwa mara, lakini hii ni kinyume cha sheria. Mara askari polisi wanapokuweka rumande ni jukumu lao kuangalia afya yako na kuzilinda haki zako. Iwapo utapata madhara yoyote au haki zako hazitaheshimiwa bali zikavunjwa kwa namna yoyote ile polisi watawajibika. Hili ni jambo muhimu la kisheria la kukumbuka.

Halafu, kutokana na ukweli kuwa askari polisi wana wajibu wa kuandika taarifa za watu wote wanaofika kituoni kwenye kitabu chao cha kumbukumbu za kila siku, kitaonesha muda ulioletwa hapo kituoni kwa mahojiano na wakati gani ulikamatwa.

Mwisho, kwa kuwa unayo haki ya kuwa na mwanasheria wako wakati wa kuhojiwa, sehemu ya mahabusu lazima ijulikane na iweze kufikiwa na mwanasheria wako, marafiki, familia au jamaa.

**80. Je, askari polisi anaweza kunishikilia kituo cha polisi au naweza kuondoka nikitaka?**

Kama umekamatwa bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazokubalika, huwezi kushikiliwa katika kizuizi kinyume cha matakwa yako. Iwapo polisi wamekuita kwa ajili ya mahojiano una wajibu wa kushirikiana nao na kuwasaidia katika uchunguzi wao. Lakini mahojiano yanapaswa kufanyika papohapo na kwa ufanisi na yasiendelee kwa muda mrefu. Kwa ujumla, kama umeshikiliwa lakini hukukamatwa, polisi wanaweza kukuhoji kwa muda wa masaa manne na siyo zaidi. Katika mazingira maalumu wanaweza kuomba kuongeza muda wa mahojiano.

**81. Iwapo askari polisi haniachilii niondoke, nifanyeje?**

Kuwekwa mahabusu bila ridhaa yako hata kwa muda mfupi ikiwa hujakamatwa kwa kufuata taratibu ni kosa kubwa. Hii inaitwa kushikiliwa kinyume cha sheria na wewe au familia yako au rafiki wanaweza kulalamika dhidi ya askari polisi huyo kwa mkubwa wake kimadaraka au kicheo au kwa hakimu. Kubwa zaidi, kupitia mwanasheria wako, familia, ndugu au rafiki unaweza kwenda moja kwa moja Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa kuomba kutolewa kwa amri ya kufikishwa kortini kuangalia uhalali wa kushikiliwa kwako ili uweze kuachiliwa mara moja. Aidha, malalamiko yako yanaweza kupelekwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi au Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.


**82. Je, askari polisi anaweza kunikamata bila kuniambia sababu?**

Hapana. Askari polisi anaweza kumkamata mtu ikiwa tu kuna sababu za kufanya hivyo. Mathalani, mtu amekamatwa papohapo akifanya uhalifu, au mazingira yote ya uchunguzi yanaonyesha kumtuhumu mtu huyo, au mtu huyo anaonekana akimsadia mtu mwingine kufanya uhalifu kabla, wakati au baada ya tukio kutokea, hivyo anaweza kukamatwa. Ni lazima kuwe na 'sababu za msingi' za kumkamata mtu. Mtu fulani kumtaja mtu mwingine katika taarifa ya awali ya upelelezi haiwezi kuwa sababu ya ukamataji. Lazima pawepo na kitu cha ziada chenye sura ya ushahidi kitakachowezesha kukukamata. Kwa bahati mbaya kuna baadhi ya watu hukamatwa isivyo halali na pasipo sababu za msingi.

**83. Je, askari polisi anahitaji kuwa na kibali ili kunikamata mimi au mtu mwingine?**

Inategemea aina ya kosa. Kuna makosa maalumu yaliyoorodheshwa katika Sheria ya Makosa ya Jinai yenye kuruhusu askari polisi kumkamata mtu bila ya hati ya ukamataji, hata hivyo makosa mengine yote yanamtaka askari polisi kupata hati ya kukamata kutoka kwa hakimu, Katibu Kata au Katibu wa Baraza la Kijiji. Endapo askari polisi watamkamata mtu bila ya kuwa na kibali, ni lazima watoe taarifa kwa hakimu kuhusu ukamataji huo.

**84. Kama polisi watanikamata bila ya kuwa na hati ya ukamataji, wanalazimika kumuarifu mtu yeyote kuwa nimekamatwa? Je, mtu huyo ataelezwa mahali nilipo?**




Ndiyo, kama polisi watakukamata bila hati ya ukamataji, lazima watoe taarifa kwa hakimu kuhusu ukamataji huo. Pia, pasipokujali umekamatwa kwa hati ya ukamataji au bila hati ya ukamataji, unayo haki ya kuwasiliana na mwanasheria, familia au rafiki yako mara baada ya kukamatwa. Unaweza kuwajulisha sehemu ulipo na sababu za kukamatwa kwako.

**85. Iwapo askari polisi wananituhumu kuwa nimefanya uhalifu, je, wanaweza pia kuwakamata wanafamilia yangu?**

Hapana haiwezekani. Hakuna hatia ya kufungamanishwa. Mtu kuwa na hatia au kukosa hatia lazima kuamuliwe kwa kuangalia vitendo vya mtu binafsi na siyo kwa sababu mtu huyo yupo karibu na au anahusiana na mtu fulani ambaye ni mtuhumiwa. Uhuru wa mtu yeyote hauwezi ukatwaliwa isipokuwa kwa sababu maalum ya sheria.

Askari polisi hawawezi kuwatisha wanafamilia au marafiki au kuwafungia mahabusu kama njia ya kumbana mhalifu akiri kosa au kama amekimbia ajisalimishe polisi. Njia hii ya kuteka na kuwashikilia watu mateka ni kinyume cha sheria na ni kosa kubwa.

Haijalishi kesi wanayoishughulikia ni ngumu kiasi gani, polisi hawawezi kutumia njia zisizo halali ili kumlazimisha mtuhumiwa kujisalimisha au kukiri kosa. Watu pekee wanaoweza kukamatwa ni wale ambao kuna sababu za msingi dhidi yao za kufikiriwa kuwa wamefanya uhalifu.

### 86. Je, kuna kanuni maalumu za kuwakamata na kuwahudumia wanawake walioko kizuizini?

Ndiyo. Upekuzi wowote wa mwanamke lazima ufanywe na askari polisi mwanamke, kwa kuzingatia heshima kwa mwanamke anayepekuliwa. Zaidi ya hayo, kila kituo cha polisi nchini kinapaswa kiwe na dawati la wanawake na watoto, lenye kusimamiwa na askari polisi waliopata mafunzo maalumu kuwashughulikia wanawake na watoto. Hivi sasa madawati haya yameanzishwa katika vituo vya polisi vya mikoa tu. Hata hivyo jitihada zinafanyika ili kuanzisha madawati hayo kwenye kila kituo cha polisi hadi ngazi ya kata.

### 87. Vipi kuhusu watoto? Je, kuna taratibu maalum kwa ajili yao?

Kama ilivyoelezwa hapo juu, kila kituo cha polisi nchini ni lazima kiwe na dawati la wanawake na watoto, lenye kusimamiwa na askari polisi waliopata mafunzo maalumu kuhusu kuwashughulikia wanawake na watoto.

Watoto wanaokamatwa wakiwa chini ya miaka 18 kwa kibali au pasipokuwa na kibali, na ambao hawawezi kupelekwa mahakamani mkuu wa kituo cha polisi ni lazima awaachilie waende kwa wazazi au walezi wao (au mtu mwingine aliye na wajibu nao). Askari polisi anaweza kuomba dhamana kutoka kwa mzazi au mlezi iwapo ataamini kuwa ni lazima kufanya hivyo ili kuwa na uhakika wa mtoto huyo kuletwa tena kituo cha polisi au mahakamani.

Hata hivyo, iwapo mtoto atakamatwa kuhusiana na mauaji, au uhalifu ambao adhabu yake ni kifungo cha zaidi ya miaka saba, au ni lazima kumweka mtoto huyo mbali na mtu asiyetakiwa basi mkuu wa kituo hatamwachilia mtoto huyo.

Aidha, watoto walio chini ya umri wa miaka 18 hawawezi kushikiliwa na polisi kwa uhalifu bila ya kumwarifu mzazi au mlezi wa mtoto huyo kuwa amekamatwa, na sababu za kukamatwa kwake. Zaidi ya hayo, watoto lazima watengwe na watu wazima, isipokuwa mtu mzima huyo akiwa ni ndugu yake. Polisi watakuwa na wajibu wa kuwatunza na kuangalia ustawi wa watoto walio chini ya uangalizi wao.

**88. Je, askari polisi wakinikamata, wanaweza kunishikilia kwa muda wowote wanaopenda?**

Hapana! Ikiwa umekamatwa na polisi na kuwekwa mahabusu bila kibali, basi askari polisi ni lazima wakupeleke mahakamani ndani ya saa 24. Hata hivyo, iwapo umekamatwa kwa kibali kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo, au umekamatwa kwa kosa na polisi hawana kibali, basi polisi lazima wakupeleke mbele ya mahakama mapema iwezekanavyo. Ikiwa hujakamatwa, lakini umeletwa kituoni kwa ajili ya kuhojiwa, basi askari polisi lazima waliweke suala hilo katika kumbukumbu zao pia.

**89. Inakuwaje basi watu hukamatwa siku ya Ijumaa jioni na kuwekwa mahabusu mpaka siku ya Jumatatu?**

Haitakiwi kuwa hivyo. Inapokuwa haiwezekani kumpeleka mtu aliyekamatwa mahakamani ndani ya saa 24 kuanzia alipowekwa mahabusu, afisa msimamizi wa kituo cha polisi ambako mtuhumiwa ameshikiliwa anaweza kuichunguza kesi na, isipokuwa kama kosa linaonekana na afisa huyo kuwa ni kubwa, anaweza kumwachia mtu huyo baada ya kuweka dhamana kwa kiasi cha kutosha akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, na kumtaka kuhudhuria mbele ya mahakama katika muda na mahali palipotajwa kwenye dhamana.

**90. Je, watu watajuaje nilipo?**

Sheria ina kinga nyingi za kukulinda usipotee ndani ya mfumo. Mara baada ya askari polisi kukukamata wanatakiwa wafanye mambo kadhaa. Lazima wachukue kumbukumbu za watu wote waliowashikilia kwa mahojiano au waliokamatwa kwa kibali au bila kibali. Taarifa za watu waliokamatwa bila kibali lazima zitolewe kwa hakimu wa eneo hilo.

Zaidi ya hayo, lazima wakufahamishe kuwa unaweza kumwarifu rafiki au nduguyo ili wajue mahali ulipo. Pia lazima wahakikishe unafahamu na unaweza mara moja kuongea na mwanasheria au mtoaji wa huduma za



kisheria. Vitu hivi vyote vimewekwa kisheria kupunguza uwezekano wa askari polisi kutumia madaraka yao vibaya. Iwapo askari polisi hawafuati taratibu hizi watatakiwa wajibu mashtaka mbele ya mahakama.

### 91. Je, ni kitu gani huandikwa ninapokamatwa?

Askari polisi lazima waweke kumbukumbu wakieleza jina, muda, tarehe, mahali ulipokamatwa, sababu za kukamatwa na kosa ambalo kila mtu waliyemkamata anatuhumiwa kulifanya.

### 92. Nitawezaje kujua yote haya?

Kisheria, wakati unapokamatwa askari polisi anatakiwa kukujulisha haki zako zote. Pia kuna taasisi nyingi ambazo zinaweza kukusaidia kujua haki zako, kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Taasisi zinazotoa msaada wa huduma za kisheria pia zinaweza kukusaidia iwapo hujui haki zako za kisheria.

### 93. Je, askari polisi anaweza kunipiga niwapo kizuizini?

Hapana. Hawezi kukupiga, kukutisha au kukutia hofu. Kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za kipolisi, na askari polisi anayefanya hayo anaweza kuadhibiwa kwa kosa hilo.

Sheria inasema kuwa mtu akiwa kizuizini, atatakiwa kutendewa kiubinadamu na kuheshimiwa na hatapaswa kutendewa ukatili, kinyume na ubinadamu au kudhalilishwa. Pia iwapo uko katika kizuizi cha polisi, unaweza kuomba kupatiwa matibabu au ushauri kuhusiana na ugonjwa au majeraha uliyonayo.

### 94. Je, askari polisi anaweza kunilazimisha kukiri kosa?

Hapana. Askari polisi anayo haki ya kukuhoji, lakini hawezi kukulazimisha kuongea kitu chochote ambacho huna habari nacho, kitu chochote ambacho hutaki kukisema au kukiri makosa ambayo hukuyafanya. Ungamo la kosa linalofanywa mbele ya askari polisi kwa namna yoyote ile halitakubalika mahakamani kama ushahidi.

### 95. Je Polisi wanalazimika kunukuu kila mahojiano wanayoyafanya na mtu baada ya kumkamata?

Ndiyo, wakati wa mahojiano Polisi analazimika kuandika maswali aliyouliza na majibu yake, maelezo mengine ya ziada ambayo umeyatoa, endapo polisi alitoa angalizo kuwa taarifa yoyote utakayoitoa inaweza kutumika mahakamani kama ushahidi dhidi yako na muda aliokueleza hivyo. Pia

anatakiwa kunukuu muda wa kuanza na kumaliza mahojiano hata kama yalisimama kwa muda kwa sababu ya mambo mengine.

Polisi analazimika kukuonyesha alichoandika ili uweze kusoma, kama huwezi kusoma, askari polisi aliyeandika maelezo hayo lazima akusomee. Unaweza kufanya masahihisho katika maelezo yako na ukisha jiridhisha kuwa maelezo hayo ni sahihi unaweza kutia saini. Kama maelezo ni marefu zaidi ya ukurusa mmoja utalazimika kutia saini kila ukurasa. Hii itazuia maelezo yako kubadilishwa na mtu mwingine baada ya kutia saini.

## 96. Je, nikiwa nashikiliwa kituo cha polisi naweza kupata dhamana?

Inategemea umekamatwa kwa kosa gani na iwapo askari polisi aliyekukamata alikuwa na hati ya kukukamata. Polisi lazima wakujulishe kuwa unayo haki ya kupata dhamana kwa mujibu wa sheria. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inasema kuwa unayo haki ya kupata dhamana ya polisi kama:

a) Utakubali kwa maandishi kuhudhuria mbele ya mahakama katika muda na mahali palipotajwa;

b) Utakubali kwa maandishi kuzingatia masharti yatakayotajwa;

c) Mtu mwingine anayekubalika na polisi anakiri kwa maandishi, kwamba anakufahamu na anaahidi kuwa unaweza kuhudhuria mahakamani kujibu mashtaka;

d) Wewe au mtu mwingine anayekubalika na polisi, anakubali kulipa kiasi fulani cha fedha kama dhamana iwapo utashindwa kuhudhuria mahakamani kujibu mashtaka;

e) Wewe au mtu mwingine anayekubalika kwa polisi, anaweka polisi, kiasi fulani cha fedha ambacho kitarudishwa iwapo utaweza kuhudhuria mahakamani kujibu mashtaka katika muda uliotajwa.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai pia inasema kuwa askari polisi msimamizi wa kituo cha polisi anaweza kumwachia mtu kwa dhamana (kiasi cha fedha kitakachorejeshwa baadaye - mojawapo ya njia zilizotajwa hapo juu), kwa kuhudhuria mbele ya mahakama katika tarehe iliyopangwa kama:

a) Ulikamatwa bila kibali;

b) Baada ya uchunguzi wa kina, kwa maoni yake, msimamizi wa kituo cha polisi ataona kuwa hakuna ushahidi unaojitosheleza kuendelea na mashtaka;

c) Kosa unaloshitakiwa kwalo siyo kosa kubwa; au

d) Inaonekana kwamba uchunguzi zaidi utatakiwa kufanywa, na hauwezi kukamilika ndani ya muda mfupi wa kawaida.

**97. Je, ni kitu gani kitatokea iwapo askari polisi ataninyima dhamana?**

Iwapo askari polisi atakunyima dhamana ni lazima auweke uamuzi wake katika maandishi na aeleze sababu za kukunyima dhamana. Zaidi ya hayo, lazima upelekwe mbele ya hakimu haraka iwezekanavyo – lakini siyo zaidi ya saa 24, au kikao cha kwanza cha mahakama. Kama uko kizuizini ukisubiri kupelekwa mbele ya hakimu unaweza kumwomba askari polisi kukuwezesha kufika mahakamani ili uweze kuwasilisha ombi lako la dhamana kwa hakimu. Kama askari huyo hatekelezi hilo, bado ni lazima akupeleke mbele ya hakimu ndani ya saa 24.

**98. Je, askari polisi anatakiwa kuangalia vitu gani anapoamua iwapo aniachilie kwa dhamana ya ahadi ya maandishi au ya kulipa kiasi fulani cha fedha?**

Askari polisi msimamizi wa kituo lazima aangalie uwezekano wa wewe kufika mahakamani kwa kurejea historia yako, kazi yako, hali ya familia na kumbukumbu zilizoko polisi kama vitu hivi vinajulikana. Pia askari polisi lazima aangalie mazingira ya kosa unalotuhumiwa kutenda, ukubwa wa kosa hilo na iwapo jamii itahitaji ulinzi. Mwisho, askari polisi lazima pia aangalie utalazimika kukaa muda gani kama dhamana haitatolewa, na mahitaji yako ya kuwa huru ili ukutane na wanasheria ili wakusaidie katika shtaka lako na mahitaji mengineyo utakayokuwa nayo kwa ajili ya ulinzi.

**99. Je, askari polisi wanawezaje kufanya kazi zao za kuwakamata wahalifu kukiwa na masharti mengi kiasi hiki?**

Awali ya yote siyo kazi ya askari polisi kuamua nani mwenye hatia na nani asiye na hatia. Askari polisi kazi yao ni kukamata na kuwashikilia watuhumiwa na washitakiwa. Lakini hawatakiwi kuwachukulia watuhumiwa kama tayari wana hatia na kuwa wanayo haki ya kuwaadhibu. Hiyo ni kazi ya mahakama. Wakati huo huo, watu walioko mahabusu lazima wapewe ulinzi dhidi ya mashtaka ya uwongo na mateso. Hii ndiyo maana kuna 'masharti' mengi. Kwa kweli siyo masharti kabisa, bali ni taratibu zilizotengenezwa ili kuhakikisha kuwa kila mmoja anayo nafasi sawa mbele ya mahakama.

**100. Mbona kuna haki nyingi kwa mshtakiwa? Vipi kuhusu waathirika?**

Watu wengi wanafikiri kuwa hakuna anayewajali waathirika wa vitendo vya kihalifu. Kwa kweli nguvu zote za Serikali ni kwa ajili ya kumsaidia mwathirika. Ni kwa niaba ya waathirika vyombo vya dola vinawatafuta wahalifu. Pia ni kwa niaba ya waathirika serikali inawaweka waendesha mashtaka kuwatetea mahakamani. Vile vile ni kwa niaba ya waathirika serikali inawaadhibu wakosaji. Lakini mtuhumiwa anasimama peke yake. Anaweza asiwe na hatia kabisa. Hivyo kuhakikisha kuwa nguvu ya vyombo vya dola

dhidi ya mtu mmoja anayetakiwa ajitetee mwenyewe, sheria imeweka kinga na vyombo kama huduma ya bure ya msaada wa huduma za kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo.

**101. Je, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina jukumu la kufuatilia nguvu na mamlaka ya polisi?**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni taasisi huru ya Serikali, iliyoanzishwa kama taasisi ya kitaifa iliyo kitovu cha kukuza na kulinda haki za binadamu na wajibu na utawala bora nchini Tanzania. THBUB ilianzishwa chini ya ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na ilianza kazi tarehe 1 Julai, 2001 baada ya kupitishwa kwa Sheria Na. 7 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001. Kulingana na kifungu cha 6(1) cha sheria hiyo pamoja na mambo mengine, Tume ina majukumu ya kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kutoa mapendekezo. Iwapo mapendekezo hayo hayakutekelezwa, inaweza ikapeleka masuala hayo mahakamani. Aidha, Tume hutoa mapendekezo kuhusu urekebishaji wa sheria iliyopo au inayotarajiwa kutungwa, kanuni au utaratibu wa kiutawala ili kutilia maanani masuala ya haki za binadamu na utawala bora.



# Vyeo vya Jeshi la Polisi Tanzania




Inspekta Jenerali wa Polisi (Inspector General of Police - IGP)




Kamishna wa Polisi (Commissioner of Police - CP)




Naibu Kamishna wa Polisi (Deputy Commissioner of Police - DCP)




Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (Senior Assistant Commissioner of Police - SACP)




Kamishna Msaidizi wa Polisi (Assistant Commissioner of Police - ACP)




Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (Senior Superintendent of Police -SSP)




Mrakibu wa Polisi (Superintendent of Police - SP)




Mrakibu Msaidizi wa Polisi (Assistant Superintendent of Police - ASP)




Mkaguzi wa Polisi (Inspector of Police - INSP)

# Vyeo vya Jeshi la Polisi Tanzania




Mkaguzi Msaidizi wa Polisi (Assistant Inspector of Police - A/INSP)



Mnadhimu wa Kambi (Regimental Sergeant Major - RSM)



Stesheni Taji (Station Sergeant - SSGT)



Sajenti (Sergeant - SGT)



Koplo (Corporal)

Commonwealth Human Rights Initiative
B-117, Iind Floor, Sarvodaya Enclave,
New Delhi – 110 017
Tel: +91 –(0)11 4318 0200;
Fax: +91 –(0)11 2686 4688
E-mail: info@humanrightsinitiave.org
Website: www.humanrightsinitiative.org

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: http://www.chragg.go.tz

British
High Commission
Dar es Salaam